PHILADELPHIA GAS WORKS
800 W. MONTGOMERY AVENUE
PHILADELPHIA, PA 19122-0050

Tarehe:
Namba ya Akaunti:
Jina la Mteja:
Anwani ya Nyumba:

# HUDUMA YAKO YA GESI IMEFUNGWA

**TUMEFUNGA HUDUMA YAKO YA GESI KWA SABABU:**

_____ Hukuturuhusu tufikie mita yako.
_____ Hukutimiza masharti na/au kutuma ombi la kushughulikia huduma.
_____ Wizi au kuharibu kifaa cha huduma.
_____ Ulaghai/Udanganyifu mkubwa.

**ILI UREJESHEWE HUDUMA YAKO LAZIMA UFANYE YAFUATAYO:**

- Ulipe Ada ya Kurejeshewa Huduma ya $123.23 (Pamoja na $372.00 ikiwa tulichimba barabara ili kufunga gesi).
- Ulipe Ada (ikiwa inahitajika) ya $_______________

Lazima uwasiliane nasi baada ya kulipa ili tuhakikishe umetimiza masharti yote ya kurejeshewa huduma na tupange jinsi ya kufika nyumbani kwako. Unaweza kutakiwa kulipa zaidi ya kiasi kilichowekwa kwenye taarifa hii ili urejeshewe huduma yako.

**TAARIFA YA DHARURA YA KIMATIBABU**

**TUFAHAMISHE** IKIWA KUNA MTU ANAYEISHI NYUMBANI KWAKO AMBAYE NI MGONJWA SANA AU ANA UGONJWA UTAKAOZIDI KUTOKANA NA KUFUNGWA KWA HUDUMA HIYO. TUTAREJESHA HUDUMA YAKO YA GESI NDANI YA SAA 24 wakati wa ugonjwa huo **mradi:**

1. Daktari mwenye LESENI msaidizi wa daktari au muuguzi anayetibu wagonjwa atathibitisha kwa maandishi kuwa ugonjwa huo upo na kuwa unaweza kuzidi ikiwa huduma yako itasimamishwa; na
2. Utatupigia simu kwa 215-235-1777 na kuweka mpango wa kulipa bili zako za huduma.
3. DAKTARI WAKO MWENYE LESENI, MSAIDIZI WA DAKTARI AU MUUGUZI ANAYETIBU WAGONJWA ATATUMA BARUA KWA PGW NDANI YA SIKU 3 INAYOTHIBITISHA UGONJWA HUO.

Ikiwa wewe ni mwathiriwa wa dhuluma na una amri iliyotolewa na mahakama, unaweza kupata ulinzi na taratibu maalum za matibabu ya dharura. **Piga simu kwa PGW mara moja kwa 215-235-1000 utufahamishe ili uweze kupata ulinzi na taratibu hizi maalum**. Tutahitaji utupatie nakala ya amri ya mahakama.

**JAMBO MUHIMU LA KUJUA**

Ikiwa una maswali au unahitaji maelezo zaidi, tafadhali tupigie simu leo kwa 215-235-1777 au ututumie barua katika P.O. Box 3500, Philadelphia, PA 19122. Baada ya kuzungumza nasi, ikiwa hujaridhika, unaweza kuwasilisha malalamiko kwa Tume ya Huduma za Umma (Public Utility Commission, PUC). Ili uwasiliane nao, piga simu kwa (800) 692-7380 au utume barua kwa: Pennsylvania Public Utility Commission, Box 3265, Harrisburg, PA 17105-3265.

- Ikiwa una amri halali ya **Kulindwa Kutokana na Dhuluma** au amri iliyotolewa na mahakama inayotambulika katika Jimbo hili inayothibitisha wazi kuwa wewe ni mwathiriwa wa dhuluma za nyumbani, unaweza kupata ulinzi wa ziada. **Tupigie simu mara moja kwa 215-235-1000**. Tutahitaji utupatie nakala ya amri hiyo na bado tutahitaji uturuhusu tufikie mita yako.

- Tupigie simu ikiwa bili yako hulipwa na mwenye nyumba. Una ulinzi fulani wa kisheria.
- Ikiwa unatatizika kuelewa au kuzungumza Kiingereza, tafadhali tupigie simu kwa 215-235-1777 ili upate huduma ya ukalimani bila malipo.
- Tafadhali wasiliana nasi ikiwa wewe ni mlemavu na unahitaji usaidizi.
- Tutahitaji uturuhusu tufikie mita yako ili tukurejeshee huduma na unaweza kuhitajika kulipa ada zozote zilizoidhinishwa za kurejesha huduma yako.
- Watu wote wazima wanaoishi nyumbani, ambao majina yao yapo kwenye makubaliano, mkataba wa kukodisha au mkopo wa nyumba wanachukuliwa kuwa mteja na wana jukumu la kulipa ili kurejeshewa huduma.

- Mtu YEYOTE mzima ambaye amekuwa akiishi nyumbani anaweza kulazimika kulipa bili yote au sehemu ya bili hii ili arejeshewe huduma.
- Tunaweza kuchukua hadi siku saba kukurejeshea huduma.